JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS - TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MVOMERO
SHULE YA SEKONDARI LUSANGA

P.O.Box 150
Lusanga –Turiani
Morogoro – Tanzania
Phone: +255655738944
+255787738944
E-mail lusangasec1990@gmail.com

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI **11/01/2021**

…….

…….

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

Ninafurahi kukuarifu kwamba mtoto wako amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021.
Shule ya Sekondari Lusanga ipo umbali wa Km 2.5 kaskazini Magharibi mwa Mji mdogo wa **MADIZINI – TURIANI**, wilaya ya MVOMERO mkoa wa MOROGORO.

Ni shule ya mchanganyiko wasichana na wavulana kwa kidato cha kwanza hadi cha nne na ina wasichana pekee kwa kidato cha tano hadi cha sita. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021, Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 22/01/2021.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1. SARE ZA SHULE

A**: WAVULANA**:

(i) Mashati meupe 2 ya mikono mifupi ya tetroni
(ii) Suruali 2 rangi ya KIJANI “ESTEM NAMBA 01”. (usishone “modo”)
(iii) Soksi jozi 2 nyeusi zisizo na urembo wala doa lolote.
(iv) Viatu nyeusi jozi 2 vyenye gidamu (kamba) na visigino vifupi.
(v) Sweta la kijani.
(vi) Tai rangi ya kijani.

B: WASICHANA:

(i) Shati 2 nyeupe za tetroni zenye mikono mifupi.
(i) Sketi 2 ndefu za KIJANI “ESTEM NAMBA 01”. zenye rinda za kawaida. (ipite kifundo cha mguu)
(ii) Hijabu nyeupe (Juba) isiyo na urembo, nusu kanzu nyeupe na sketi ndefu kwa wasichana wa kiislamu) kitambaa cha Hijabu ni tetroni. Hijabu iwe na urefu wa kufika kiunoni.
(iii) Tai rangi ya kijani
(iv) Viatu jozi 2 nyeusi vyenye gidamu (kamba) na visigino vifupi.
(v) Sweta la kijani.
(vi) Soksi jozi 2 nyeupe zisizo na urembo wala doa lolote.

C: SARE ZA MICHEZO:

- Sare ya michezo kwa shule hii ni Truck suit rangi ya bluu bahari kwa wasichana na wavulana.
- Raba zenye gidamu.

2: MAHITAJI YA DARASANI ANAYOPASWA KUWA NAYO.

- Kalamu za kutosha
- Daftari kubwa za kutosha 11 (Counter book)
- Penseli za kutosha
- Mkebe wa vifaa vya Hisabati
- Dictionary (Kamusi ya Kiingereza-kiingereza)
- Rula/mstari
- Graph paper
- vitabu

3: VIAMBATANISHO:

1. Fomu ya kukubali masharti: Fomu hii ijazwe na Mwanafunzi pia na Mzazi au Mlezi na kuikabidhi shuleni.
2. Kivuli cha cheti cha kuzaliwa
3. Uthibitisho wa afya: peleka fomu iliyoambatanishwa kwa Mganga Mkuu wa Mkoa au Wilaya SIYO ZAHANATI ili upimwe afya na fomu irudishwe shuleni.

5.0: SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE:

5.1: Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu na: 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na: 10 ya 1995 Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais - TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya Msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yako mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) HESHIMA kwa viongozi, wazazi na wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni JAMBO LA LAZIMA.

(b) MAHUDHURIO mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

(c) Kushiriki kwa makini kutimiza maandalio ya jioni (preparation)

(d) KUWAHI katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa

(e) Kufahamu MIPAKA YA SHULE na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa Uanafunzi wako katika shule hii.

(f) Kutunza USAFI WA MWILI NA mazingira ya shule

(g) Kuvaa sare ya shule WAKATI WOTE UNAPOTAKIWA.

(h) Kuzingatia RATIBA YA SHULE wakati wote na

(i) Kutunza mali za umma.

5.2: MAKOSA YAFUATAYO YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE:

a) Wizi.
b) Uasherati na Ushoga.
c) Ubakaji

d) Ulevi wa matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, kokeni, Mirungi, Kubeli na kadhalika.
e) Kupigana au Kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
g) Kudharau Bendera ya taifa
h) Kuwa mjamzito au Kupata mimba.
i) Kuoa au kuolewa
j) kutoa mimba
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au
l) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Kumiliki simu ya mkononi,line,charger,redio na vinavyofanana na hivyo.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

MUHIMU:

- **Zingatia kitambaa cha kushona sketi na suruali kiwe ni kijani esteem No.1 ambacho kimeambatanishwa pamoja na fomu hii na si vinginevyo.**
- **Siku ya kuripoti kila mwanafunzi aambatane na mzazi/mlezi wake,kwa atakayekuja bila mzazi/mlezi hatopokelewa.**

KARIBU SANA LUSANGA SEKONDARI

BAHATI M. OMARY
MKUU WA SHULE

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI LUSANGA

TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI NA KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA

PICHA

A: TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI:

- JINA LA MWANAFUNZI ……
- TAREHE YA KUZALIWA……
- MAHALI ALIPOZALIWA (MKOA/WILAYA) ……
- MAHALI ANAPOISHI (KATA/MTAA) .....
- DINI YAKE NI.....DHEHEBU.....
- URAIA …….
- SHULE ALIYOTOKA…….
- NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI NI.....NA.....
- NAMBA YA MTIHANI/USAJILI DARASA LA SABA……..

B: TAARIFA YA MZAZI:

- JINA LA MZAZI/MLEZI……
- MZAZI YUPO HAI/HAPANA …….
- KAZI YA MZAZI/MLEZI ……
- BABA NA MAMA WANAISHI PAMOJA? NDIO /HAPANA …….
- ANUANI YA MZAZI/MLEZI ……..
- SIMU YA MZAZI/MLEZI (tafadhali andika namba zinazotumika na mhusika kama ni mama au baba n.k)
  …… ……..
  ……

C: KUKUBALI NAFASI NA MAELEKEZO ULIYOPEWA (MWANAFUNZI)

Mimi ……. Kidato ……mwaka…… Nimesoma na kuyaelewa yote. Kwa hiyo nakubali kuipokea/sikubali kuipokea nafasi niliyopewa. Nathibitisha kwamba nimepokea maagizo au maelekezo bila kulazimishwa kuyazingatia.

Tarehe ……. Saini ……

D: **KUKUBALI SHERIA ZA SHULE :(MWANAFUNZI)**
Mimi …… nimezisoma na kuzielewa sheria za shule na nina ahidi kwamba nitazingatia na kutii masharti, sheria za shule na maelekezo mengine nitakayopewa na walimu na viongozi wote wa shule, nikikiuka sheria hizo hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu kwa mujibu wa kanuni, taratibu na sheria zilizopo.

Tarehe …… Saini…….

MEDICAL CERTIFICATE EXAMINATION

(To be completed by medical officer in respect of FORM I/V Entrants)

Student full Name ……

Age…….. (years)

Blood count (red and white)…….

Stool examination ……..

Urine analysis ……..

Syphilis Test ……

Eye test …….

T.B test …….

Ears ……..

Chest…….

Spleen …….

Abdomen ……..

ADDITIONAL INFORMATION: age physical defects or impairments infections, chronic or family diseases ect.

I certify that the above named student is fit/unfit for admission into a day/boarding Secondary School.

Signature…….

Designation ……

Station ……

Date ……